

Mpango wa ruzuku ya pembejeo za kilimo na matumizi mabaya ya fedha za umma

Vifurushi vya Mpango ya Ruzuku ya Pembejeo za Kilimo (FISP) unafadhiliwa na serikali za nchi husika ili kuwasaidia wakulima wadogo. Lakini vocha na mbolea mara nyingine huibiwa na mara kadhaa huelekezwa kwa wafanya biashara na wakulima wakubwa.

Kuna **uwazi mdogo** sana kuhusu mikataba ya mbegu na mbolea, hivyo ni vigumu kupiga mahesabu ya kiasi cha fedha za umma ambacho makampuni ya mbegu na mbolea



yanapokea. Mifumo ya ufuatiliaji na tathmini ni dhaifu au haipo, na haijulikani ni kiasi gani cha mbolea na mbegu kinapotea.

Katika mipango mingi ya ruzuku ya pembejeo za kilimo Kusini mwa Afrika, pembejeo za ruzuku huwa zinaibwa kabla ya kusambazwa (njia ya mchepuko), na wanufaika hukombo vocha kwa fedha taslimu au kuuza vifurushi vya ruzuku zao kwa wengine (kuvuja).

- ▶ **Tanzania** – 60% upotevu wa mbolea kwa njia ya mchepuko.
- ▶ **Zambia** – 35% njia ya mchepuko au kuvuja kwa pembejeo.
- ▶ **Malawi** – 33% chepushwa au vujishwa katika masoko ya pili.
- ▶ **Afrika Kusini** – kiasi kikubwa cha pembejeo kimechepushwa na kuuzwa kwa wakulima ndani ya nchi au kusafirishwa nje ya mipaka kimagendo.